

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



CHUO CHA MAJI



Tarehe: 06/11/2020

TAARIFA KWA UMMA

SEKTA YA MAJI WASHAURIWA KUKITUMIA CHUO CHA MAJI KUPATA HUDUMA ZA KITAALAMU

Watendaji Wakuu na watumishi wa taasisi za Wizara ya Maji mkoani Singida, wameagizwa kukitumia Chuo cha Maji katika kupata huduma za kitaalamu zinazohusiana na Sekta ya Maji baada ya kufungua tawi mkoani wa Singida.

Hayo yalisemwa na Naibu Katibu Mkuu, Wizara ya Maji Mhandisi Nadhifa Kemikimba alipokuwa kwenye mkutano wake na watumishi wanaofanya kazi katika taasisi za Wizara ya Maji zikiwemo, Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Singida (SUWASA), Wakala wa Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA) mkoa wa Singida, Bodi ya Maji ya Bonde la Kati, na Maabara ya Ubora wa Maji mkoa wa Singida.

Mkutano huo ulitanguliwa na kikao kazi cha Maafisa Habari wa Taasisi zote za Wizara ya Maji uliofanyika katika ukumbi wa Bodi ya Maji ya Bonde la Kati.

Pamoja na hayo, Chuo Cha Maji kimeagizwa kuendelea kutoa huduma zenye tija na ubora kwa wataalam wa sekta ya maji kwani wataalamu hao wana mchango mkubwa katika kutimiza lengo la serikali la kuwahudumia wananchi nchini ili huduma za maji zimfikie kila Mtanzania.

Kitengo cha Mawasiliano